# Watoto wenye ulemavu wanastahili kuthaminiwa

■ Na Grace Gurisha

MTOTO anatakiwa kuongozwa katika njia sahihi ambayo itamwelekeza kuishi maisha safi ya kumnufaisha yeye na kizazi chake kwa kuzingatia maadili, mila na tamaduni stahili kwenye jamii husika.

Kati ya malezi ambayo mtoto anatakiwa kupewa ni kutakiwa kuwaheshimu wakubwa azingatie adabu, staha na unyenyekevu kwa kila mtu ambaye amemzidi umri na hata ambaye wanalingana.

Maadili ni uwezo wa mtu kutambua na kutenda ipasavyo katika jamii anayoishi, mtoto anapozaliwa hajui mema wala mabaya bali anajengewa maadili kutokana kwa kufundishwa na wazazi na watu walio karibu na familia yake.

Wazazi na walezi wanapaswa kuwa na mwitikio chanya ili kumwezesha mtoto kuwa na maadili kuanzia nyumbani na kwa jamii.

Vivyo hivyo kwa watoto mwenye ulemavu wanahitaji upendo na kulelewa katika mazingira yasiyo na migogoro ili nao wajione kuwa wanahaki ya kuishi kama wanavyoishi wenzao ambao hawana




Watoto wakiwa wamekalishwa kwenye baiskeli zilizotolewa msaada na Kampuni ya Utafiti na Uchimbaji wa Madini ya Montero. Wapili kushoto ni Meneja Mkuu wa Montero, Grant Pierce.Wanne kushoto ni Mke wa Rais wa awamu ya tatu, Mama Anna Mkapa ndiye aliyekabidhi baiskeli hizo. (PICHA NA MPIGAPICHA WETU)

wapo baadhi ya ... wanaona kuwa ukiwa na mtoto mlemavu ni mkosi, na kusahau kuwa mtoto yeyote ambaye amekuwepo katika dunia yupo kwa makusudi maalumu na ameletwa na Mwenyezi Mungu hivyo kumwadhibu mtu kutokana na ulemavu wake si sahihi.

Tatizo hili linawakumba baadhi ya wanawake ambao wamejifungua watoto wenye ulemavu, ambapo waume zao huwa wanawakimbia kwa kuona kuwa mtoto huyo ni mkosi.

Wanawake wengi wenye watoto wenye ulemavu wamekuwa wakilalamikia tatizo la kukimbiwa na wazazi wenzao, mmoja wa wanawake hao ni Mama Stumai.

Mama Stumai anasema kuwa wakinababa wengi wamekuwa wakikimbia watoto wao kutokana na ulemavu waliyokuwa nao nakuona kuwa hawawezi kuwasaidia katika maisha ya mbeleni.

Anasema kuwa asilimia kubwa ya wanaume wamekuwa wakiwakimbia wake zao na kuoa mwanamke mwingine bila kujua kuwa mtoto huyo anayemkimbia yeye hakumuomba Mungu ampatie mtoto mwenye mapungufu.

Hata hivyo anasema kuwa wakinababa wengine wamefikia hatua ya kuwafukuza wake zao manyumbani kwa kuona kuwa hastahili kuishi nyumba moja.

Mama huyo aliyasema hayo Septemba 15 mwaka huu Dar es Salaam, katika Kijiji cha Makumbusho wakati wakipokea msaada wa baiskeli.

Msaada huo wa baiskeli ulitolewa na Kampuni ya Utafiti na Uchimbaji wa Madini ya Montero, ilitoa baiskeli 55 kwa watoto wenye ulemavu.

Kwa furaha bila kusita kuonesha hisia zake anasema kuwa watu wengine wanaochangia wao kunyayaswa kisa wanawatoto walemavu wamekuwa wakitolewa maneno ya kashfa ili kuona kuwa ukoo wao umepata mkosi.

Anasema Wakwe wamekuwa tatizo sana katika ndoa zao,licha ya kupata matatizo makubwa kutoka kwa waume zao nakuwaona wao hawafai katika jamii.

"Mtoto mwenyewe hata umlee kwa miaka 20 bado hakui, sasa huyo mtoto wa aina gani kama siyo anapoteza muda, ... kwa kumnukuu maneno ya mama Mkwe.

Mama huyo anasema kuwa Wakwe watambue kuwa hata watoto wao wanaweza wakapata ajali na wakapata ulemavu kwa sababu Mungu ndiyo anapanga na sio binadamu.

Hata hivyo aliomba Serikali kuwachukulia hatua wanaume wote wanaokimbia wake zao kwa sababu ya kujifungua watoto walemavu, limekuwa ni tatizo sugu.

"Wanaume hao wamekuwa wakifanya kama mchezo wa kuigiza kwa sababu wanaona hawachukuliwi hatua yoyote ya kisheria, naomba Serikali utumie nguvu kuwa tia hatiani", anasema.

Vile vile anasema kuwa wapo taayari kutoa ushirikiano wa aina yoyote ile ili wakamatwe na kutiwa hatiani, kwa nia ya kukomesha tabia hiyo.

"Hapa leo tumekusanyika wanawake 55 ambao watoto wetu wanaulemaavu, lakini nusu ya akinamama wameachwa na waumezao", anasema.

Baiskeli hizo zilikabidhiwa na mke wa Rais Mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, Mama Anna Mkapa katika Kijiji hicho.

Kampuni hiyo kwa ... msaada huo,kwa sababu anasema wakinamama wengi walikuwa wakipata shida kwa kuwabeba watoto wao migongoni.

Mama Mkapa ambaye ni mwanzilishi na Mwenyekiti wa Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF) anasema baiskeli zitawasaidia migongo yakina mama kupumzika.

Hata hivyo anasema anaziomba Manispaa wanapojenga majengo kama Shule wawakumbuke watoto wenye ulemavu, kwa sababu wengi wanakuwa wakipata shida kutokana na aina ya jengo lilivyojengwa.

Naye Meneja Mkuu wa Montero Tanzania, Grant Pierce anasema baiskeli hizo zimetengenezwa maalum kwa ajili ya watoto walemavu katika Shirika lisilo la Kiserikali "Wheelchairs for Kids" la nchini Australia.

"Baiskeli hizi zitaleta utofauti kati ya kuudhuria ama kutohudhuria shule,kuwa sehemu ya jamii au kutengwa, tunafurahia kuwa sehemu ya furaha yao", anasema Pierce.

Pierce anasema jumla ya baiskeli 160 zimeletwa Tanzania ili kusambazwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kampuni ya Montero ni kampuni inayojihusisha na uchimbaji wa madini na maendeleo ya kampuni iliyojiunga nayo ya Wigu Hill Eath Elements (REE).

Anasema REE inayofanya mradi wake Tanzania na Kampuni zingine za madini za Tanzania, Afrika Kusini na Quebec Canada.

Alibainisha kuwa baiskeli hizo zinatengenezwa zinatengenezwa nchini Australia na wafanyakazi wastaafu wanaojitolea na mpaka sasa ina nguvu kazi ya watu 100.

Pierce anasema wastaafu hao wanatengeneza, wanahakiki viwango, kupanga na kupakia kwenye maboksi, wafanyakazi wengine wa kujitolea wanatengeneza foronya na wanasesere.

Tangu kuanzishwa kwake imetoa baiskeli kwa maelfu ya watoto wanaoishi na ulemavu nchini Australia, Afrika na Asia.

Naiomba jamii iwachukulie watoto walemavu kama watoto wengine, pia Serikali ijitaidi kuwasaidia wakiona mama wanaokimbiwa na waume zao kwa kuwachukulia sheria.

0718 030337.